JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MKOA WA SIMIYU,
Simu Na: 0753 321 860
Baruapepe: info@simiyurrh.go.tz

WIZARA YA AFYA

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA,
S.L.P 17,
BARIADI - SIMIYU

Kumb Na: AB108/292/01A/13

28/11/2025

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA KUJITOLEA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, inatangaza nafasi za ajira za kujitolea kwa kada Mbalimbali kwa muda wa mwaka Moja, kama ifuatavyo;

NA	KADA	NAFASI
1.	Afisa Habari Msaidizi	1
2.	Wasaidizi wa Afya	6

1. AFISA HABARI MSAIDIZI II DARAJA LA II (ASSISTANT INFORMATION OFFICER GRADE II) - Nafasi 1

1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukusanya na kuandika habari;
ii. Kupiga picha za mnato;
iii. Kupiga picha za video;
iv. Kuandaa picha za maonyesho;
v. Kutunza picha/maktaba na marejeo;
vi. Kuandaa majarida na mabango (Posters);
vii. Kukusanya takwimu mbalimbali zinazohusu habari; na
viii. Kuandaa majarida na vipeperushi.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Dilpoma ya Uandishi wa Habari au sifa zinazolingana na hizo kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali, awe na ujuzi wa kutumia kompyuta

2. MSAIDIZI WA AFYA- TGHOS A NAFASI 6.

2.1 Sifa za mwombaji.

Awe amehitimu kidato cha nne waliopata mafunzo ya mwaka mmoja katika mafunzo ya afya.

2.2 **Kazi na majukumu.**

i. Kufanya usafi wa vifaa vya kazi, usafi wa wodi, na mazingira.
ii. Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza katika kwenda haja (Kubwa na ndogo) na kuoga.
iii. Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiejiweza.
iv. Kuchukua nguo za mgonjwa kuzipeleka kwenda kufuliwa.
v. Kuchukua sampuli za mgonjwa kwa ajili ya vipimo vya maabara na kufuatilia majibu.
vi. Kutayalisha vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufunga majeraha.
vii. Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa.
viii. Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

3. MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI.

Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa za jumla kama ifuatavyo

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na umri usiozidi miaka 45.
iii. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea (Cheti cha kidato cha Nne, Sita, Taaluma na Usajili kamili) "Full Registration" au Leseni hai ya kufanya kazi ya taaluma husika.
iv. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la Jinai au kufungwa jela.
v. Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji (CV).
vi. Maombi yaambatishwe na nakala ya vyeti vya Elimu, Taaluma na Cheti cha Kuzaliwa.
vii. Malipo ya Mshahara yatakuwa 50% ya Mshahara wa ngazi wa kuanzia Kada husika kwa watumishi wa serikali.
viii. Testimonials Results Slips **HAZITAKUBALIWA**.

Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 24/12/2025

Maombi yatumwe kwa;

Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Simiyu,
S.L.P 17,
BARIADI-SIMIYU.
Au tuma kwa barua pepe: info@simiyurrh.go.tz

Imetolewa na;

Dkt. Athanas K.Ngambakubi

MGANGA MFAWIDHI

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SIMIYU

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA
YA MKOA - SIMIYU